

NANI MWANAMKE?

Aina 6 Za Wanaume Zisizowavutia Wanawake

(Kitabu cha Pili)

Na

Shamte Kilalile

Contents

HAKIMILIKI	3
KIDOKEZO.....	1
UTANGULIZI	3
SURA YA KWANZA.....	5
SURA YA PILI.....	9
SURA YA TATU.....	14
SURA YA NNE	18
SURA YA TANO	21
SURA YA SITA	24
HITIMISHO.....	27
MUHTASARI	28
KUHUSU MWANDISHI.....	29
KAZI ZINGINE ZA SHAMTE KILALILE.....	30

HAKIMILIKI

Hakimiliki© 2023 Shamte Juma Kilalile

Haki zote zimehifadhiwa. Kwa malipo ya gharama husika umeruhusiwa kusoma kitabu hiki. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupakua au kusambaza bila idhini ya kimaandishi kutoka kwa Mwandishi. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa atakayekiuka.

Yaliyomo kwenye kitabu hiki yametokana na fikra na mawazo ya Mwandishi na wala yasitumike kama sehemu ya ushauri wa kisheria au binafsi. Ni jukumu lako kuchunga mwenendo na tabia zako binafsi.

Shamte J. Kilalile

Kijichi, Dar Es Salaam

Tanzania

KIDOKEZO

“A way to a woman’s heart is through her emotions” (njia ya kuuteka moyo wa mwanamke ni kupitia hisia zake).

Ni maneno yangu yaliyokuwepo kwenye kitabu changu cha kwanza cha **Aina 8 Za Wanaume Zinazowavutia Wanawake**.



Katika kitabu kile nilisema wanawake ni viumbe vyenye hisia zaidi kuliko wanawake na sababu pekee inayowafanya wanaume aina zile 8 kuwavutia zaidi wanawake kuliko wanaume wengine ni kwasababu **wanagusa hisia zao ambapo ndipo udhaifu wao ulipo**. Kama hujakisoma kitabu cha *Aina 8 Za Wanaume Zinazowavutia Wanawake* ni vizuri ukaanza nacho kwani msingi wa kitabu hiki cha pili unachokisoma sasa ulianza kule.

Kitabu hiki **Aina 6 Za Wanaume Zisizowavutia Wanawake** ni upande mwengine wa shilingi wa wanaume ambao **wanazivuruga na hawajui kuzigusa hisia** za wanawake. Nimekiandika mahususi kwa ajili ya;

1. Kumuonyesha mwanaume kama hakujiona kwenye kitabu cha kwanza cha *Aina 8 Za Wanaume Zinazowavutia Wanawake* bila shaka anaweza kuwa kwenye aina hizi kwenye kitabu hiki cha pili.
2. Wanaume ambao huambulia ‘vibuti’ kila wanapotongoza wanawake hivyo hujihisi kuwa hawana bahati.
3. Wanaume ambao hawadumu kwenye mahusiano au ndoa zao. Kila akiwa na mwanamke baada ya muda tu mahusiano au ndoa huvunjika.

UTANGULIZI

Kwa umuhimu wa utangulizi huu ambao niliandika kwenye kitabu changu cha kwanza, nimeona kuna umuhimu wa kuanza na sehemu ya utangulizi ule kwenye kitabu hiki pia. Aidha nimeufanyia mabadiliko kidogo ili kukidhi lengo la kitabu hiki.

Nani mwanamke?

Hakuna jibu la moja kwa moja la swali hili kwasababu majibu yake inategemea ni nani anayeuizwa na katika mazingira gani swali hili limeulizwa. Baadhi ya majibu ni;

1. wapo wanaume wanaosema mwanamke ni chombo cha starehe,
2. wapo waandishi waliondika vitabu na kusema ni kiumbe kisichoeleweka na
3. wapo wanaharakati wasemao ni kiumbe chenye nguvu na jasiri mwenye uwezo wa kufanya sawa na anayoyafanya mwanaume.

Licha ya utofauti huu wa majibu, wote tunakubaliana ya kuwa kimaumbile na namna walivyoumbwa, **wanawake ni viumbe vya kihisia (*emotion creatures*) zaidi kuliko wanaume.** Ikiwa wote tunakubaliana katika hili, hii inajulisha ya kuwa;

1. wale wanaume wanaosema wanawake ni chombo cha starehe wakiwa wanajihalalishia kukidhi hisia na haja zao tu, kauli hii itakuwa ya kimakosa kwa sababu wanawake nao wana haki hiyo kama wao na zaidi kwa sababu ya maumbile yao.
2. wale wanaosema ni kiumbe kisicholeweka, kwa upande mmoja kauli yao itakuwa ya sawa kwasababu hisia ni kitu chenye kubadilikabadilika na wanawake hisia zao zinabadilikabadilika kutegemea na hali na mabadiliko katika miili yao. Mfano mwanamke huwa katika hisia tofauti akiwa kipindi cha ujauzito na siku zao za mwezi.

Lakini upande mwingine, wameshindwa kuelewa na kuisoma saikolojia ya mwanamke inavyofanya kazi katika hisia zake. Mfano kuna wakati mwanamke anaweza akasema hapana lakini akimaanisha ndio na kuna wakati akasema hapana akimaanisha hapana. Kuzijua nyakati hizi kunawapa shida wanaume wengi ndio maana kunaleta kauli mfano wa hii ya kusema ni viumbe visivyoeleweka.

3. ama kuhusu kauli ya wanaharakati, mimi ninaamini kama ambavyo kuna mambo ambayo mwanaume hawezi kuyafanya sawa na mwanamke kadhalika kuna mambo mwanamke hawezi kuyafanya sawa na mwanaume. Na utofauti huu unatokana na maumbile yao ambayo Mungu amewauumba na kumfanya kila mmoja kumtegemea mwenzake.

Na kila ambaye atajaribu kwenda kinyume na kanuni hii atajiletea madhara kwake mwenyewe au kwa familia yake hata kama atajitutumua na kujidai mbele ya kamera, magazeti na vyombo vingine vya habari kuwa anajivunia kuwa hivyo. Nitaishia hapa katika kuwajibu wanaharakati kwa sababu sio lengo la kitabu hiki kufanya hilo.

Inaweza kuwa ngumu kumuelewa mwanamke kwa ujumla wake lakini ni rahisi kumvunjavunja katika vijishehemu mbalimbali na kumuelewa kutegemea na vijishehemu hivyo kwa kuwa msingi wa kauli tuliyokubaliana ya **mwanamke ni kiumbe chenye hisia** inatupa mahali pa kuanzia.

Katika kuifata na kusimama katika kauli hii ndio nimeandika kitabu hiki cha pili **Aina 6 Za Wanaume Zisizowavutia Wanawake** kuelezea vipi hisia za mwanamke zinamfanya kuwachukia au kutovutiwa na aina hizi.

Ninatumai kupitia kitabu hiki mwanaume yoyote atakaejikuta yupo kwenye mojawapo ya aina hizi atachukua hatua za;

1. kubadilisha tabia zake ili kudumisha ndoa na mahusiano yake na mke au wake zake.
2. Kubadilisha tabia zake na kuwa mwanaume mwenye bahati ya kupata mke wa ndoto zake na kusahau 'vibuti'

Ungana nami.

SURA YA KWANZA

RAFURAFU

(Unattractive)



Mwanaume rafurafu ni mwanaume ambaye hajali usafi wake. Ni mchafu kwenye mwili wake, mavazi yake, nywele zake, mazingira yake anayoishi na kulala, kinywa chake, chakula chake na kila sehemu.

Kuna aina mbili za wanaume rafurafu;

1. Urafurafu unaotokana na shida za kimaisha
2. Urafurafu wa kujitakia au tabia zao.

Dhumuni la sura hii ni kuelezea aina ya pili.

Ushawahi kumuona mwanamke anavyozungushazungusha macho yake kuangalia mazingira ya geto au nyumba yako siku ya kwanza anapofika kwako? Kama anafanya hivi nyumbani kwako, elewa kuwa anafanya hivi kwa kila mwanaume anayemtongoza kwa mara ya kwanza. Anaangalia hali ya nywele zake, shati lake, mkanda wake kadhalika suruali na viatu. Ndani ya muda mfupi tu ashapata jibu la kumpa. Unaweza kufanya jaribio la kumsogelea mwanamke kama unataka kumuuliza kitu halafu angalia macho yake yalivyo haraka kukuangalia kuanzia juu mpaka chini (*scanning*).

Wanawake wanapenda kuona wanatongozwatongozwa kwasababu inawapa ile hisia ya **‘bado yuko sokoni’** kwa hiyo hata kama atakuwa kashapata jibu la kumpa mwanaume, atamsubiri kwanza aanze kumwaga ‘sera’ zake. Lakini pia kitendo cha kusubiri mwanaume aanze

kumtongoza, anajaribu kuangalia jibu ambalo aliliandaa kwa ajili yake ni sahihi au alimfikiria vibaya. Changamoto iliyopo kwa wanaume rafurafu hawapati hata nafasi ya kufikia hatua hii ya kusikilizwa sera zake kutokana na muonekano wao.

Linapokuja suala la jinsia hizi mbili kila mmoja kulala au kutolala na mwenzake, mwanaume na mwanamke wanatofautiana namna wanavyoangaliana na kutoa maamuzi katika hilo. Mwanaume anapomuona mwanamke huwa anamuangalia kwa ujumla wake (*looking for general*) kuwa **‘huyu ni mwanamke’** kisha **anakiangalia kinachomvutia** kama ni wowowo, sura au kingine chochote. Akikipata anafanya maamuzi ya kumtongoza. Akikosa anaweza kuacha au akaamua tu kutongoza kama jaribio kwasababu ni katika hulka ya mwanaume kutongozatongoza. Akikubaliwa, atalala nae si kwa sababu anampenda bali kukidhi haja zake. Mwanaume anapoamua kukidhi haja zake huwa ajali hali ya huyo mwanamke kama ni rafurafu au lah. Wewe unadhani ni nani ambaye anawapa ujauzito wale wanawake wanaozurura mitaani ambao wamepata mitihani ya kurukwa akili? Jibu, ni wanaume ambao wameamua kukidhi haja zao bila kujali hali za wanawake hao.

Hali iko tofauti kwa wanawake. Mwanamke anapomuona mwanaume anayemtongoza huwa anaangalia **kwa umahususi yaani kitu kimoja kimoja peke yake** (*looking for specific*), **hukipa maksi kila kimoja** na **kufanya maamuzi ya kumpa nafasi ya kuingia hatua nyingine au hapana**. Sasa hebu fikiria unamfata mwanamke mdomo wako unanuka kwa ugoro/milungi/hujapiga mswaki, shati lina rangi ya njano makwapani linalotokana na jasho lako na suruali chafu, unategemea utapata jibu gani? Utafukuzwa kama mbwa koko.



KWANINI RAFURAFU HAMVUTII MWANAMKE?

1. Sababu inayofanya mwanaume rafurafu asipate hata nafasi ya kusikilizwa sera zake hata kidogo ni kwasababu anazizima (*turning off*) na kuzivuruga hisia za mwanamke. Mwanamke anapomuangalia mwanaume juu mpaka chini (*scanning*) anatafuta majibu ya ya harakaharaka ya maswali haya mawili kichwani mwake;
 - anaendana na mimi? (*is he my type?*) na
 - tunaendana tukiwa pamoja (*do we look good together?*)

Kwa hiyo mwanaume rafurafu anapomtongoza, anawaza hivi mashoga zake siku wakijua amelala na mwanaume wa hali hiyo au yuko kwenye mahusiano nae, uso wake atauweka wapi. Tofauti na mwanaume, mwanamke hata hamu zake zimshike vipi hawezi kulala na mwanaume rafurafu hata kwa *one-night standing*.

Mwanamke pekee atakayehusiana na mwanaume rafurafu ni aidha awe kahaba mwenye shida ya kupata pesa au mlevi chakali au yule anayefanana naye kimuonekano yaani rafurafu kama yeye. Fatilia wale watumia madawa ya kulevya (mateja) na wale wanaohusiana nao, utagundua ni wao kwa wao.



2. Wanaume wanavutiwa na wanawake kwa kuwaona wakati wanawake wanavutiwa na wanaume kupitia milango yote ya fahamu/hisia (*sensory organs*); macho (kuona muonekano wake mzuri), masikio (kusikia maneno mazuri), ulimi (kuonja chakula kwa mwanaume anayejua kupika), ngozi (kugusa mwili wa mwanaume) na pua (kunusa harufu nzuri ya mwanaume). Kwa hiyo mwanaume rafurafu hamvutii mwanamke kwa harufu yake wala muonekano wake.

NINI CHA KUFANYA KUTOKUWA RAFURAFU?

1. Muonekano wako ndio sababu ya kupigwa ‘vibuti’ kila mara. Jitahidi kujiweka nadhifu kwa usafi wa mwili wako, mavazi na mazingira unayokaa. Kuwa nadhifu si kujikalifisha kununua vitu vya gharama nje ya uwezo wako. Mfano nguo, inatosha kuzifua, kuzipiga pasi na kuzivaa kwa mpangilio.
2. *First impression matters* ikiwa na maana ya kuwa kuna umuhimu mkubwa sana namna unavyojiwasilisha kwa mwanamke kwa mara ya kwanza. Ukiwajisilisha kama mwanaume rafurafu usiyejali usafi wako ndivyo mwanamke atakavyokuchukulia na kuona kuwa ndiyo tabia yako. Badilika.

SURA YA PILI

MTOTO WA MAMA

(Mama's Boy)



Mtoto wa Mama ni aina ya mwanaume ambaye hawawezi kufanya maamuzi mwenyewe katika **KILA KITU** mpaka amuulize mama yake (*seeking approval from his mother*) au kupata muongozo kutoka kwa mama yake. Mama akisema hapana, hafanyi na akisema ndio, anafanya. Mfano; mke wake akimuomba hela kwa ajili ya matumizi fulani ya kikike, mwanaume aina hii atamuuliza mama yake kama ampe au asimpe. Akipanga mipango ya kimaendeleo na mkewe, atamuuliza mama yake anaionaje mipango yao atekeleze au asitekeleze.

Sababu kuu inayofanya jamii kuwa na wanaume wa aina hii ni kupatikana wakina mama ambao wamelea watoto zao wakiume toka kipindi wakiwa wadogo katika mifumo mikuu miwili;

1. Mfumo wa mama mtawala (*controlling mother*) na
2. Mfumo wa 'mama anajua zaidi' (*mama knows better*)

Matokeo ya mifumo hii imewafanya watoto hawa kushindwa kufanya maamuzi yao wenyewe hata kwenye masuala madogo ya kawaida kipindi cha utoto wao na wanakuwa katika hali hiyo mpaka ukubwani mwao na kuja kuathiri mahusiano yake na mkewe.

Na vyanzo vya kupata wamama wa aina hii ni vitatu;

1. Wakina mama ambao wana nguvu na wako juu ya waume zao kisauti katika ndoa zao na kuwalea watoto zao katika mifumo hiyo.
2. Wajane au wakina mama walioachwa ambao baada ya vifo vya waume zao au kuvunjika kwa ndoa zao walichukua jukumu la ulezi asilimia 100 katika mifumo hii wakiamini inafaa.
3. Aidha kuumizwa na wanaume katika mapenzi au kufata fikra ya kiharakati iliyoibuka kwenye jamii. Sababu hizi zinafanya siku hizi kuibuwa wanawake wanaotaka kuzaa nje ya ndoa na kulea watoto wao wenyewe bila baba zao. Wanajiita wenyewe ni SUPER WOMEN (Wanawake wa Nguvu).

Kuna umuhimu mkubwa mtoto kulelewa na wazazi pande zote mbili. Mtoto wa kike anapolelewa na baba na mama anapata kitu fulani katika elimu kinachohusiana na uwanamke kutoka kwa mama yake na jinsi ya kuishi na mwanaume kadhalika anajifunza kitu kutoka kwa baba yake kuhusu tabia za wanaume kwa wanawake na jinsi gani mwanaume aishi na mke wake.

Kadhalika mtoto wa kiume akilelewa na wazazi wake wote, anapata kitu katika kuwaonea huruma wanawake ambayo inakuja kumsaidia siku akija kuoa. Upande wa baba, anapata kitu katika uvumilivu wa kimaisha, utoaji wa maamuzi, mamlaka na uthubutu wa kiume.

Kwa hiyo mtoto wa kiume akilelewa na BABA TU anaweza kupata mojawapo kati ya haya;

1. huwenda akaja kuwa mtu wa mabavu sana atakapokuja kuwa mkubwa AU
2. kwa kudra za Mungu na ulezi mzuri wa baba, anaweza akakua vizuri na kuwa mwanaume bora.

Kadhalika akilelewa na MAMA TU;

1. kuna uwezekano akaangukia kuwa na tabia za kikekike AU,
2. kama ilivyo kwa baba, naye kwa kudra za Mungu na ulezi wake mzuri, kijana anaweza akakua vizuri na kuwa mwanaume bora AU
3. kuwa ‘mtoto wa mama’ ambaye ndio kusudio la sura hii.

KWANINI MTOTO WA MAMA HAMVUTII MWANAMKE?

Uwezo (*authority*) na nguvu ya kutoa maamuzi (*dominance*) kwa wanaume ni katika sifa zinazopatika miongoni mwa aina za wanaume niliowaandika katika kitabu changu cha kwanza cha *Aina 8 Za Wanaume ni Zinazowavutia Wanawake*. Mtoto wa mama anakosa sifa hizi.

Tabia ya mwanaume aina ya Mtoto wa Mama kutaka muongozo kutoka kwa mama yake katika KILA KITU kinachohusiana na maisha na mahusiano yake na mkewe ndio sababu inayofanya mwanamke kutovutiwa naye.

Mtoto wa Mama yupo katika kundi la wanaume ambao ndoa zao au mahusiano yao huvunjika ndani ya muda mfupi. Tofauti na mwanaume aina ya rafurafu ambaye anakataliwa na mwanamke kabla ya mahusiano kuanza kutokana na muonekano wake, mwanaume aina ya Mtoto wa Mama anapata fursa ya kutongoza na kusikilizwa sera zake na kama mwanamke akivutiwa naye basi anakubaliwa. Changamoto ni kuwa tabia hii ya utoto wa mama si rahisi mwanamke kuijua wakati anapotongozwa na mwanaume wa aina hii mpaka baada ya kuingia kwenye mahusiano. Tabia inapoendelea, mwanamke anashindwa kuivumilia hatimaye anavunja mahusiano haraka sana.

NINI CHA KUFANYA KUTOKUWA MTOTO WA MAMA?

1. Yajue ni mambo gani unatakiwa kuyachukulia maamuzi kama mwanaume na mambo gani yanafaa kuomba watu ushauri (mama akiwa miongoni wa hao watu).
2. Mke na mama kila mmoja ana haki na daraja lake kwako. Mpe kila mmoja haki yake na muke kila mmoja kwenye daraja lake. Hauwi mtoto wa mama ukimpa daraja na haki anayostahili mama yako.

Kuna swali linapenda sana kuulizwa katika suala linalohusiana na mwanaume aina hii ambalo naona kuna haja nami kulijibu. Swali lenyewe ni **je kati ya mama na mke ni nani anafaa kukaa kiti cha mbele cha gari langu?** Yametumika maneno ‘kiti cha mbele cha gari’ kama lugha ya picha ila makusudio haswa ni kuwa ni nani anapaswa kupewa kipaumbele kati ya mke na mama.

Kwa hiyo yawezekana hauna gari lakini kuna mambo ambayo unaweza kukutana nayo ambayo yatakutaka utoe kipaumbele kwa mmojawapo kati ya wanawake hawa muhimu maishani mwako. Swali ni kuwa ni yupi basi utanza nae?

Majibu yanategemea misimamo ya watu na wapi wamechukua misimamo hiyo. Misimamo ya watu inatoka katika vyanzo vitatu;

- a) **Akili:** Kutokana na elimu zao kuna watu wanaona inatosha kutoka na misimamo yao kwa kutumia akili zao **TU**,
- b) **Mifumo:** mfano imani za kidini na fikra mbalimbali kama za kiharakati,
- c) **Matamania ya nafsi:** Kuna watu wanapenda kuchukua msimamo utakaofurahisha nafsi zao kwasababu ya maslahi. Kiasili kila mwanadamu ana akili na mfumo fulani anauofata kwenye maisha yake uwe wa kidini, kiharakati au mwengine. Watu wa matamania wakilipata jambo huwa wanalichanganua baina ya akili zao na mifumo wanayoifata kisha wanatoka na misimamo itayofurahisha nafsi zao.

Mfano katika ndoa ya wake wengi katika imani ya dini ya kiislamu, mume anapokufa wake zake wote wana haki ya mirathi **SAWA** bila kujali mke mmoja ameolewa miaka 15 iliyopita na mwengine ameolewa jana (*isipokuwa ikiwa kuna uwekezaji ulifanyika katika biashara mfano mume na huyu mke aliyeolewa miaka 15 iliyopita walichangia kila mmoja wao asilimia fulani katika mtaji kama vile nusu kwa nusu, mume akifariki huyu mke atachukua asilimia yake na asilimia ya mume iliyobaki itagawiwa SAWA baina ya wake wote kama nilivyosema hapo awali*).

Kwa hiyo kwa mwanamke mwenye kufata matamania ya nafsi, sheria hii haingii akilini kwa mwanamke aliyeolewa miaka 15 iliyopita apate mirathi sawa na mwanamke aliyeolewa jana. Atakachofanya mwanamke huyu ni kukataa sheria ya kiislamu huku akisema inamuonea (matamania ya nafsi) na kutaka mirathi igawiwe kwenye mahakama ya kiserikali (maslahi ya kupata haki zaidi kwa sababu ya miaka yake 15 aliyoishi na mume wake). Na kinyume chake, sheria hii ya kiislamu itakuwa nzuri upande wake ingekuwa yeye ndiye mwanamke aliyeolewa jana.

Kwa hiyo kujibu swali hili; **je kati ya mama na mke ni nani anafaa kukaa kiti cha mbele cha gari langu?** Mimi ni katika watu ambao misimamo yangu naichukua katika dini kwasababu naamini aliyeumba dunia hii na kila kitu ndani yake akiniambia fanya jambo fulani atakuwa yuko sawa haijalishi inaingia akilini mwangu au hapana. Ikiwa aliyetengeneza gari akituambia gari hili linatumia mafuta ya petroli hatuthubutu kuweka mafuta ya diesel kwasababu tunamuamini na tunajua tutaharibu gari tukienda kinyume nae. Sasa iweje Mungu tusimuamini kwa kiasi hiki na zaidi?

Na kama mtu akiamua kudadisi kwa kina kila kitu ambacho Mungu amekikataza au kukiamrisha kukifanya, atakuja kugundua kinaaingia akilini. Anachotakiwa kukifanya ni kuieka fikra zake huru bila kufata matamanio ya nafsi yake na kutenga muda kudadisi suala husika.

Kwa hiyo katika dini ya kiislamu **mama ana nafasi kubwa kwa mtoto wake kuliko mke**. Kupata pepo na kuridhiwa kwa mtoto wa kiume kuko chini ya mama yake wakati mwanamke anapoolewa mambo hayo yako chini ya mume wake (haaingii akilini eenh? Hahaha).

Chunguza kila ndoa ambayo kuna mwanamke amefanya juhudi mume wake agombane na mama yake ili mapenzi yote yawe kwake, matokeo ni kuwa mwanamke huyo amekosa alichokitaka. Kisha chunguza kila ndoa ambayo kuna mwanaume alikuwa amegombana na mama yake kisha mke alifanya juhudi kumpatanisha mama na mwanae, mke alipata mapenzi kutoka kwa mume na mkwe. Kwa hiyo kwangu mimi mama yangu anakaa siti ya mbele labda atake yeye kukaa nyuma.

Sikatai kuna wakwe ni vivuruge kwenye ndoa za watoto wao na uislamu umefundisha wanaume namna ya kuisha na mama wa aina hii bila kuwavunjia heshima na daraja zao. Ni mada ndefu lakini inatosha mpaka hapa kwa dhumuni la kitabu na kujibu swali husika.

3. Jinasue kutoka katika makucha tegemezi ya mama. Ni jambo gumu kwasababu ni kitu ambacho umelelewa toka udogoni mwako ila inawezekana. Kila jambo mwanadamu akiamua kulifanya, analiweza. Kuna watu waliamua kuacha pombe na madawa ya kulevya na wakaweza sasa kwanini wewe usiweze kujinasua?

SURA YA TATU

GUBU

(Argument Man)



Gubu ni mwanaume ambaye haishi kulalamika au kutoa kasoro katika kila kitu ambacho mke wake anafanya au kumfanyia. Kama kuna wanaume ambao wanawake wanawachukia na kukereka nao basi ni wa aina hii.

Utawajua kwa mfano wa kauli hizi;

1. “Chakula hakina chumvi kabisa. Ungeweka kama kile cha jana kingekuwa kizuri” (*hicho chakula cha jana anachikiiiongelea, jana hiyo alikitoa kasoro kwa kusema hakijaiva*)
2. “Madirisha yana vumbi kama nini, sijui unafanyaje usafi wewe mwanamke”
3. “Ngoja nifanye mimi leo usafi naona watu wanalipualipua tu” (*siku hiyo amemua kufagia kikorido na wala sio nyumba nzima anatoa shombo hizo fikiria siku akifagia nyumba nzima itakuaje. Na siku hiyo ya kufagia nyumba nzima haitakuja kutokea, mdomo tu ndio unawasumbua*).
4. “Hawa watoto wanakaa na kula bure tu hakuna lolote wanalolifanya” (*shombo kwa mke aliyemuoa akiwa na watoto ambao sio wake*)
5. “Ndio nini sasa? Mbona unatisha?” (*shombo kwa mke aliyejipamba usiku kwa ajili ya kumfurahisha mume wake. Fikiria itamkata stimu kiasi gani mwanamke huyu*)

Kama ilivyo kwa mwanaume aina ya Mtoto wa Mama, si rahisi kwa mwanamke kumjua mwanaume Gubu mpaka baada ya kuwa nae kimahusiano. Ndoa za wanaume aina hii zina matokeo manne;

1. Kuvunjika baada ya mwanamke kushindwa kuvumilia tabia yake.
2. Mwanamke kuchepuka ili kupata kile anachokikosa kwa mwanaume huyu mfano kuambiwa maneno mazuri, kujaliwa na mapenzi.
3. Kumchuna kama mwanamke anaona kuna maslahi zaidi anayapata kwa mwanaume wa aina hii. Akifikia tu lengo lake, anaaachana nae.
4. Kuuliwa. Wanaume hawa wana maneno makali yanayochoma hisia za wanawake mpaka wanawake wengine wanafikia hatua ya kuwaua kwa kukusudia au bila kukusudia.

Hebu fikiria mwanamke ambaye ameamua siku hiyo anunue kivazi fulani cha mtego kisha ajipambe haswa kwa dhumuni la kumfurahisha mumewe usiku. Kutahamaki mwanaume huyo anakuja kumwambia, “Ndio nini sasa? Mbona unatisha?”, bila shaka kama kuna kitu karibu huyu mwanamke anaweza kukichukua na kumpiga nacho kwa hasira,



KWANINI GUBU HAMVUTII MWANAMKE?

1. Kwasababu ya maneno ya shombo yenye kuwachoma hisia zao. Kama ambavyo mwanamke anavutiwa na mwanaume mwenye kuzigusa hisia zake kadhalika anamchukia mwanaume ambae anaumiza hisia zake.



2. Wanaume wenye gubu hawathamini mchango na juhudi za wake zao katika chochote. Mwanamke akijitahidi kupika vizuri anakosolewa, akijitahidi kuvaa vizuri anakosolewa. Kama ilivyo kwa binadamu yoyote kupenda kuthaminiwa mchango wake kwenye familia, kazini au biashara, mwanamke nae kama binadamu anapenda kuona mumewe anathamini mchango wake anaoufanya kwake.

Maneno kama “chakula kitamu mke wangu, ahsante” au “umependeza mke wangu mashaAllah, kwani tuko *honeymoon* nini? (unatania kidogo), maneno haya yana maana kubwa sana kwa mwanamke.

Ajabu ya kuwa mwanaume mwenye gubu bosi wake kazini asipotambua mchango wake analalamika mpaka koo linamkauka.

NINI CHA KUFANYA KUTOKUWA MWANAUME MWENYE GUBU?

1. Usiwafanyie watu kitu ambacho kama ungefanyiwa wewe usingependa. Jaribu kuvaa viatu vya mkeo kwa kujiuliza hivi “ingekuwa mimi nimejifukiza manukato vizuri kwa ajili ya mke wangu kisha aniambie ninanuka, nitajisikiaje?”. Vaa viatu hivyo kwa kujiuliza maswali katika kila nyanja kama chakula, mavazi na usafi.

2. Jifunze kuwa na maneno mazuri ili usiwe sababu ya mkeo kuchepuka au kukutia kilema cha kurushiwa stuli kwa sababu ya gubu lako.



3. Thamini mchango anaoufanya mkeo kwako, nyumbani na familia kwa ujumla. Mfano umerudi kwenye mzinguko yako ya kutafuta riziki na umegundua kuna mabadiliko yamefanyika sebureni, usijifanye kauzu bali onyesha umetambua na kumsifia kwa akichokifanya (wanawake wanapenda kubadilishabadilisha mandhari nyumbani utakuta sofa hili wamepeleka huku lingine kule na mfano wa hilo)

SURA YA NNE

MASHAUZI

(*Bragging Man*)

Mwanaume mashauzi ni aina ya wanaume ambao wanapenda kujisifia wana vitu au sifa fulani. Utawatambua kwa kauli zao kama hizi;

1. “Mimi nina pesa chafu mrembo, nikubalie nibadilishe Maisha yako”
2. “Kama ushawahi kusikia mwanaume mashine, basi hiyo mashine ninayo mimi”
3. “Ukinikubalia mrembo jua utakuwa kimahusiano na mtu mwenye digrii peke yake nchi nzima kutoka Harvard”
4. “Nitakupeleka siku moja kwenye jumba langu la kifahari lilopo pembezoni mwa bahari kule Kigamboni”

Kuna aina mbili za wanaume mashauzi;

1. **Muongo:** Huyu ni yule ambaye anajisifu kwa vitu au sifa ambazo hana. Lengo lake ni kujionyesha kwa njia ya kumhadaa mwanamke ili ampate. Mwanaume aina hii kama alijishau kwa utajiri kama mfukoni akiwa na milioni 1 au 2 ataipoteza kwa vinywaji na vyakula kwa mwanamke ili tu kuthibitisha uwongo wake.

Mtego wanaopenda kuutumia wanawake kuwabaini wanaume hawa ni mdogo sana. Badala ya kuhadaika na vinywaji na vyakula ambavyo ndio lengo la mwanaume huyu, wanawake wanatangaza shida zao zingine kabisa mfano atamuomba mwanaume huyu pesa nyingi kutegemeana na utajiri aliojidai nao. Mfano ataomba milioni 5 za mtaji wa biashara. Rungu hili litamfanya mwanaume huyu kuingia mitini huku akilalamika bia, nyama zake kuliwa na tabia ya wanawake wa siku hizi kuomba pesa siku ya kwanza tu ya kutongozwa bila kujua kuwa mwenye kosa ni yeye mwenyewe.

2. **Mkweli:** Huyu ni yule ambaye anachojigamba nacho ni kweli anacho. Na hata akiombwa milion 5 anaweza kutoa hapohapo. Tatizo ni kuwa mwanaume mashauzi mwenye sifa ya ukweli akifaulu mtego wa kuombwa pesa anakuwa bado hajamaliza viunzi vya kuruka kwani kwenye kichwa cha mwanamke anawekwa kwenye kundi la wanaume wa kuchunwa kwa kitendo chake cha kujionesha yeye tajiri.

KWANINI MASHAUZI HAMVUTII MWANAMKE?

1. Sifa ya kujishaua ni sifa za kike na kila mwanamke mwenye kujielewa hapendi kuiona sifa hiyo akijipamba nayo mwanaume wake. Mwanaume mashauzi mwenye sifa ya ukweli tuliyemuona hapo juu hatimaye hufanikiwa kuingia kwenye mahusiano na mwanamke lakini mahusiano haya huwa hayadumu. Sababu ni kuwa mwanamke ataanza kujaribu kumbadilisha tabia yake ya umashauzi kwa kauli kama hii, “hivi unajua unaniabisha sana hebu achana na hii tabia yako bwana”.

Nina uhakika asilimia 99.9 hawa wanaume wenye tabia za kishauzi maarufu kama CHAWA lazima wanapata kauli hizi. Kama si kuambiwa kuacha basi ataambiwa apunguze ikiwa mwanamke ataona uchawa wa mume wake ndio unawaweka hapa mjini.

2. Mwanamke anamjua mwanaume mwenye kitu fulani bila ya mwanaume huyo kujitangaza. Kama huamini jaribu zoezi hili;
 - kusanya wanawake wachache kuanzia wawili mpaka watano kisha waambie kuna kazoezi kidogo unataka wakusadie.
 - Waambie zoezi lenyewe ni kuwa utawapeleka sehemu na gharama za vinywaji ni juu yako ila unataka tu wakuambie mtazamo wao kwa kila mwanaume atakayeingia kwenye sehemu hiyo (unaweza kuchagua wakuambia wanaume 10 tu kama *sample*). Wanawake wanapenda ofa na kwa kuwa ushawaahidi vinywaji ni juu yako, watakubali tu.
 - Wakikubali kila mmoja mpe *notebook* au kijitadftari
 - Kisha tafuta sehemu kama mgahawa au hoteli kisha kaeni mahali ambako kutawapa nafasi ya kuona mlangoni kila anayeingia.
 - Kila mwanaume ambaye ataingia na ungetaka kujua mtazamo wao waambie wanamuonaje mwanaume huyo kwa kukuandikia kama wanaweza kuwa na mwanaume huyo kimahusiano na sababu zao.
 - Baada ya kumaliza zoezi linganisha walichoaandika kwa kila mwanaume. Utashangaa

Baadhi ya sababu ambazo unaweza kuzipata; ni muonekano wa kimwili wa wanaume hao, hali za kiuchumi, hisia juu ya tabia zao na wengine wanaweza kwenda mbali kukuandikia hata hali ya saizi ya maumbile ya viungo vyao vya kiume . Kama mwanamke anaweza kuyajua haya kwa kumuangalia tu mwanaume, sasa fikiria kuna mwanaume mashauzi anakuja na kujishaua mbele yake kwa sifa kedekede ambazo anaweza kuzihisi kwa macho yake.

Kujishaua kwa mwanaume kunaonyesha kujishusha kwake (*low status*), udhaifu (*inferiority*) na kutafuta kukubaliwa kutoka kwa wengine (*seeking approval from others*). Hizi ni sifa za mwanaume goigoi na mwanamke havutiwi na mwanaume goigoi,

NINI CHA KUFANYA KUTOKUWA MWANAUME MASHAUZI?

1. Muache mwanamke agundue mwenyewe sio wewe ujishaue mbele yake. Kimaumbile wanawake wanapenda kudadisidadi wanaume zao. Ukishakua mtu wa kujifaharisha kila kitu kwake hakuna tena kitu cha ajabu kwako ambacho angetamani kukijua.

Lakini hebu fikiria mwanamke anakuja kujua mwanaume aliyenaye kwenye mahusiano ni miongoni mwa wawekezaji wakubwa kwenye kampuni ya Apple kisha anamuuliza, “baby nilikuwa napitia mtandaoni nikaona jina lako. Sikujua kuwa na wewe ni miongoni mwa wawekezaji wa kampuni ya Apple”. Halafu kidume kinajibu, “ndio sikuona kama ni **ishu** sana kukuambia, kwani umechukia mpenzi?”.

Nakuhakikishia asilimia 99.9 ya wanawake hakuna atakayejibu amechukia. Anaanzaje kumchukia muwekezaji wa Apple ambaye sio ‘**ISHU**’ kwake kufanya mambo kama hayo. Sanasana atauliza kama kuna kampuni nyingine kubwa ambayo amewekeza au ataendelea kudadisi kama kuna kitu gani kingine cha kuvutia (*interesting*) alichonacho mpenzi wake.

2. Kama ambavyo wanaume hawavutiwi na wanawake mwenye sifa za kiume (*tom boys*) kadhalika wanawake hawavutiwi na wanaume wenye kujipamba na sifa za kike. Badala yake wanamchukulia mwanaume wa namna hii kama mwenzao (shoga yao). Mwanaume jipambe na sifa za kiume hakuna haja ya kujifanisha na wanawake. Kama Mungu angeona kuna haja ya wewe kuwa mwanamke asingeshindwa kufanya hivyo.

SURA YA TANO

MWANAUME ASIYEJAMINI

(*Insecure Man*)

Kuna aina mbili za wanaume wasiojamini;

1. **Mwanaume wasiwasi:** Mwanaume wa aina hii haamini mwanamke aliyekuwa naye kama anampenda kweli. Kila mara akiwa mbali na mke wake anawaza anasalitiwa kwa wanaume wenye pesa zaidi yake au wenye muonekano mzuri zaidi yake.

Tabia za mwanaume wasiwasi ni hizi;

- *Kupiga simu mara kwa mara:* Akiwa mbali na mke wake hachoki kumpigia simu mara kwa mara kumuuliza mahali alipo. Kama mwanamke akimjibu yuko nyumbani, mwanaume wasiwasi atamuambia mkewe afanye chochote kuthibitisha kama yuko nyumbani kweli. Ngoja nikupe kisa kimoja cha wanaume wa aina hii.

Kuna mwanamke mmoja alipata kuolewa na mwanaume wasiwasi. Basi kila mwanaume huyo alipokuwa mbali na mke wake alimpigia simu na kumuuliza yuko wapi. Mkewe akijibu yuko nyumbani, mume huyu anamwambia awashe Brenda yao ya kutengenezea juisi kuthibitisha hilo. Kwahiyo Brenda ikawa ndio kithibitisho kikuu kiasi kwamba mpaka mwanamke akienda kupiga stori kwa shoga zake huibeba kama tahadhari. Mume akimpigia simu akiwa bado yuko huko kwa shoga zake basi anaiwashia hukohuko kwenye nyumba za watu. Shoga zake walikuwa wanacheka sana kitendo hiki na kumuonea huruma kwa shida anayopata ya kufichaficha Brenda kwenye kanga kila anapokwenda kwao.

- *Kuweka ulinzi:* Akiona kupiga simu haitoshi, anaweza kumpa kazi hata jirani yake awe anamchuguzia mkewe mwenendo wake hata kwa malipo. Kwa yule mwenye pesa ataajiri na mpiga picha kabisa.
- *Ushirikina:* Nadhani ushawahi kusikia kuna wanaume wanawawekea wake zao 'tego' ili wakichepuka tu basi yeye na mchepuko wake wanase. Anajua akipiga simu anaweza akadanganywa na akiajiri mtu atapoteza pesa nyingi kwahiyo njia inayompa amani ya moyo ni 'tego'. Kwa hiyo maadamu mkewe hajaswa kwake ni ishara ya uaminifu. Chukua kisa kingine hiki cha mwanaume aliyefanya hili kwa mkewe.

Kipindi chote cha ndoa yao mwanamke mmoja hakupata kumsaliti mume wake. Sasa kuna siku ghafla yule mume alipata ajali na kufa. Baadae huyu mwanamke alipata mahusiano mengine na mwanaume ambaye ni mganga. Siku walipoamua

kukutana ili kufanya ‘yao’, yule mganga kuna mambo akayaona hayaeleweki kwenye ‘uwanja’ wa mwanamke. Ilibidi yule mwanaume amwambie ukweli yule mwanamke kuwa yeye ni mganga na kila akiingalia ngoma anaona haichezeki. Mara moja mwanamke akajua huwenda aliyefanya hivyo atakuwa marehemu mumewe.

Yule mganga alijaribu kufanya anachoweza ili kumtegua ikashindikana ilibidi waachane ila akamshauri ahangaike kwa ‘wataalamu’ wengine la sivyo haitokuja kuwezekana yeye kuwa kimahusiano na mwanaume mwengine kwasababu watakuja kunasa na mtoaji wa mnaso kashakufa. Angalia tabu hawa wanaume wasiwasi wanayowapa wanawake zao.

2. **Mwanaume Kujitutumua:** Mwanaume mwenye kujielewa, mamlaka (*authority*) na kujiamini huwa hatumii nguvu nyingi kuyaonyesha hayo kwa mkewe au familia yake. Mkewe anajua kuwa hapa niko na ‘kidume’. Sasa aina ya pili ya wanaume wasiojimini ni wale ambao wanajitahidi sana kuonyesha uwanaume wao kwa wake zao au familia zao. Utawajua kwa kauli zao za kujitutumua na umimi mfano wa hii;
 - Siku akimkoromea mkewe utasikia, “Nasema hii ni nyumba **yangu** na **mimi** ndio baba mwenye nyumba” (*kuna namna nyingi za kumueleweshwa mwanamke kuliko kujitutumua na unachomiliki kana kwamba hajui kuwa hiyo nyumba ni yako*)

KWANINI MWANAUME ASIYEJAMINI HAMVUTII MWANAMKE?

1. Kumpigia pigia simu mwanamke na kumuwekea mtu wa kumfatilia si ishara ya upendo kwake bali ni ishara ya kutomuamini. Mwanamke akiamua kumsaliti mwanaume anaweza kufanya hilo na asijue.

Kama ni muangaliaji wa filamu, kuna filamu ya zamani sana inaitwa *The Bodyguard* iliyochezwa na Jet Lee inayoelezea Tajiri mmoja aliyemuajiri Jet Lee kama mlinzi wa kumchunga mke wake mwenendo wake. Tabia hii ilimchukiza sana yule mwanamke mpaka akawa anamshawishi Jet Lee atembea nae. Ni uaminifu tu wa Jet Lee ndio ulimfanya yule mwanamke asifanikiwe. Sasa, jiulize kuna wanaume wangapi wataweza kufanya uaminifu huo kwa mkeo unayempenda kumfatiliafatilia kila mara.

2. Kujitutumua ni ishara ya kujidogosha na mwanamke havutiwi na mwanaume anayejidogosha. Paka kwasababu ya udogo wake wa umbile akikasirika anajitutumua ili aoenekane mkubwa lakini Simba hana haja ya kufanya hivyo kuonyesha ujemadali wake. Kwa hiyo kitu chochote kinachojitutumua kiasili hicho ni kitu kidogo.

Mwanaume anapojitutumua kwa mkewe anaonyesha uhalisia wa udogo wake ambao umejificha ndani yake. Anaona kama nisipojitutumua, mwanamke atamdharau lakini ukweli ni kuwa huko kujitutumua ndio sababu ya kudharauliwa na mwanamke.

Kumbuka wanawake na wanaume tunachakata (*processing*) mambo tofauti. Jambo linaweza kuonekana kwa namna fulani na mwanaume ila kwa mwanamke ni kinyume chake mfano hili la mwanaume kujitutumua.

NINI CHA KUFANYA KUTOKUWA MWANAUME ASIYEJAMINI?

1. Kuna namna nyingi za kumuelewesha mwanamke kuliko kujitutumua na unachomiliki. Unapomuoa mwanamke *automatically* anajua kuwa wewe ni baba mwenye nyumba na hauna haja ya kulithibitisha hilo kila mara mnapopishana katika jambo fulani.
2. Wanawake hawapendi kufatiliwa kama watoto wadogo. Kama amekubali kuwa nawe ni kwamba amekupenda basi onyesha kumuamini. Angekuwa hakupendi angekutaa siku ileile uliyomtongoza na usingemfanya chochote.
3. Kauli na matendo yako hutafsiriwa tofauti na wanawake. Epuka kuonyesha ishara za kujidogosha kwa kauli zako na matendo yako.

SURA YA SITA

MUONEVU

(Bully)



Hii ni aina nyingine ya wanaume ambao matendo yao yanatafsiriwa kama ishara ya wanaume wasiojiamini. Mwanaume muonevu (*Bully*) ni aina ya wanaume ambao wanapenda kuwakandamizi watu wengine ambao wana nguvu duni kushinda yeye. Mfano jitu la miraba minne kumuonea mtu dhaifu. Ukiringanisha uwezo wa kinguvu baina ya watu hawa wawili, bila shaka mtu dhaifu hawezi kuwa tishio kwa jitu la miraba minne, kwanini sasa amuonee?

Hebu pata picha hii; mwanamke yuko matembezi na mume wake wa miraba minne kisha njiani wanakutana na mtu asiyeona. Ghafla yule mwanaume bila sababu yoyote anamsukuma yule kipofu kwenye maji machafu. Unafikiri huyu mwanamke atafurahia kitendo hichi? Jibu ni hapana na sababu ni kuwa mwanamke ni kiumbe mwenye kutawaliwa na hisia sana na hukionea huruma kila kiumbe ambacho ni dhaifu kikionewa na kiumbe chenye nguvu.

Matokeo ni kuwa baada ya kuona kitendo kile sehemu ya matembezi iliyobaki hautamsikia tena mwanamke huyu akiongea kwasababu atakuwa kwenye tafakari kubwa ya hatima yake na mahusiano na mwanaume wa aina hii. Atawaza kama iliwezekana kipofu kuonewa kiasi kile bila sababu yoyote basi kuna siku naye atakakuja kufanyiwa kitu sawa na kile.

Chanzo cha kupata wanaume waonevu katika jamii ni makuzi ya kimanyanyaso aliyopitia mwanaume huyu kipindi cha utoto wake aidha kwa baba yake mzazi au wa kambo au ndugu

wengine au jamii. Ikiwa hakupata ushauri wa kisaikolojia kukabiliana na hali hii, manyanyaso yanakuja kuwa tabia yake kwa watu wengine anapokuja kuwa mtu mzima.



Wakati mwengine sababu inaweza ikawa ni kujionyesha tu na kutaka sifa. Kuna wanaume wakiona kuna kundi la wanawake sehemu hujifanya wababe kwa wanaume dhaifu ambao amewakuta kwenye mazingira karibu na kundi hilo ili aonwe na kundi hilo la wanawake kama mwanaume ngangari. Asichokijua kwenye fikra za wanawake anaonekana na kutafsiriwa kama mpuuzi (*jerk*) badala ya ngangari kama alivyokusudia.

Nakumbuka wakati niko shule ya msingi, kuna jamaa mmoja alikuwa na tabia ya aina hii. Mpaka tunamaliza shule hakufanikiwa kumpata hata msichana mmoja wa kusingiziwa aliyejulikana kama msichana wake.

KWANINI MWANAUME MUONEVU HAMVUTII MWANAMKE?

1. *Kukosa amani moyoni:* Mwanamke hupata hisia kama mume wake huwafanyia ukatili wanaume wenzake, je yeye atasalimika vipi.
2. *Utumwa:* Mapenzi ya mwanamke kwa mwanaume muonevu yanajengeka kutoka na hofu ya kuogopa manyanyaso na si suala la kutoka moyoni kwake. Ndio maana wanawake wengi walioingia kwenye mtihani wa kuwa kimahusiano na wanaume wa aina hii ni ngumu kuachana nao. Na wakifanikiwa kuachana nao huama mji na kuishi mbali nao ikiwezekana hata majina wanayabadilisha.

NINI CHA KUFANYA KUTOKUWA MWANAUME MUONEVU?

1. Tafuta ushauri wa kisaikolojia. Kama ulishawahi kupitia manyanyaso ya kijinsia utotoni na hukupata ushauri wa kisaikoloji ni vizuri ukafanya hivyo. Mara nyingi wanaume wa aina hii ni ngumu sana kujijua kama mapito yao ndio chanzo cha wao kuwa hivyo. Na hata akijua ni ngumu kumfata mtu kuongea ili amsadie kwa sababu kufanya hivyo ni kujitia aibu na ishara ya udhaifu mkubwa kwake. Piga moyo konde na mtafute mtu unayemuamni uongee nae kwasababu tabia hiyo ikiendelea inawezekana ikaja kukufikisha kwenye mikono ya kisheria.



2. Uwanaume wa mwanaume kwa mwanamke hauthibitishwi kwa uonevu bali unathibitishwa kwa kuendana na mazingira; unakuwaje ukiwa chumbani, unakuwaje mwanaume wakati wa furaha, unakuwaje mwanaume wakati wa changamoto kama wakati wa maradhi kwa mkeo na unakuwaje mwanaume kwa watoto,
3. Kauli na matendo yako hutafsiriwa tofauti na wanawake. Epuka kutafsiriwa kama mwanaume usiyejamini kwa vitendo yako.

HITIMISHO

Kwanini sikuweka wanaume wasiokuwa na pesa kama miongoni mwa wanaume wasiovutia wanawake? Kwasababu suala la mwanaume kuwa au kutokuwa na pesa inategemea ni mwanamke gani mwanaume huyu anamtongoza na kutaka kuwa nae. Mfano mwanaume ambaye ni muajiriwa kutaka kuwa kimahusiano na mwanamke tajiri na mfanyabiashara mkubwa. Huyu mwanaume bila shaka ataonekana maskini kwa huyu mwanamke.

Lakini vipi kama akitaka kuwa na mwanamke ambaye ni muajiriwa mwenzake au na mwanamke kiwango cha chini kuliko yeye? Jibu inawezekana na yapo mahusiano ya aina hii mengi sana ya watu waliooana wakiwa kazini au ya mwanamke wa kiwango cha chini kuliko mumewe. Kwanini? Kwasababu kwa wanawake wa kiwango sawa au chini, mwanaume muajiriwa anaonekana ni mtu mwenye pesa na anayeweza kujikimu.

Kwa hiyo wanaume wanapokataliwa na wanawake ambao sio viwango vyao wanalalamika kuwa wanawake hawawapendi wanaume wasiokuwa na pesa. Mahusiano ya mwanamke tajiri au mwenye pesa na mwanaume maskini yatawezekana tu ikiwa mwanamke mwenyewe ataridhia. Na uwezekano baina ya watu hawa kukutana ni mdogo sana kutoka na mazingira yao wanayotembelea. Tajiri ana viwanja vyake na mtu wa kawaida au maskini ana viwanja vyake. Ya nini basi kusubiri mpaka ukutane na huyo mwanamke tajiri tena kwa bahati sana kisha akuridhie na umaskini wako na wakati unaweza kucheza katika viwanja vyako na ukapata mwanamke atakayeendana na wewe?

Epuka tu tabia za wanaume aina 6 nilizozitaja humu utafanikiwa kupata mwenza wako.

MUHTASARI

1. Wanawake ni viumbe vyenye hisia. Huvutiwa na wanaume wenye kuzigusa hisia zao na hukerekwa na wanaume wenye kuzitibua hisia zao.
2. Wanaume aina zote 6 hawawavutii wanawake kwasababu wanazitubua na kuzivuruga hisia za wanawake. Kama hujaliona hilo rudia tena kuzisoma
3. Wanaume wanadhani pesa inaweza kuwa sababu ya kumbakisha mwanamke lakini ukweli ni kuwa mwanamke hawezi kumvumilia mwanaume tajiri mwenye tabia ya gubu, utoto wa mama, anayemfatiliafatilia, rafurafu, muonevu au mashauzi. Ukiona mwanamke anamvumilia mwanaume mwenye tabia hizi 6, kuna asilimia kubwa sana mwanamke huyo anapata furaha yake mahali pengine. Chunguza.
4. Sio kweli wanawake hawawapendi wanaume wasiokuwa na pesa bali ishuhari ya kuwa au kutokuwa na pesa inategemea wanaume wanataka wanawake wa kiwango gani. Tafuta wa kiwango chako na epuka tabia za wanaume hawa 6 niliowataja humu utafanikiwa.

KUHUSU MWANDISHI

Shamte Kilalile anaishi Dar es Salaam, Tanzania na ni mhitimu wa shahada ya Uchumi na Mipango kutoka Chuo Kikuu Mzumbe, Morogoro. Amebobeza katika Ujasiriamali, Masoko, Uandishi wa Matangazo (*Copywriting*), Uandishi wa vitabu na Uandishi wa miswada ya filamu. Na ni mwanagenzi katika fani ya *Coding*.

Ni mwanzilishi wa SparkCopy na anatoa huduma za;

1. uandishi wa riwaya (*novels*), vitabu vya biashara/ujasiriamali au miswada ya filamu (*scripts*) kwa watu wenye stori au mawazo vichwani mwao lakini hawezi kuandika vitabu au miswada kwa ajili ya filamu wanazotaka kuzitengeneza.
2. uandishi wa matangazo ya redio, televisheni, kubrandi ukurasa wa LinkedIn, *motivation letter* au *statement of purpose* kwa wanafunzi wanaokwenda vyuo vikuu vya nje na *cv/resume*.

Kujua zaidi huduma hizi tembelea tovuti <https://sparkcopy.wordpress.com/>

Ni mtaalamu wa masoko (*marketing consultant*) na anatoa huduma kwa wafanyabiashara wanaohitaji msaada kubusti masoko kwa ajili ya biashara zao. Kujua zaidi huduma hii tembelea tovuti: <https://yourmarcon.wordpress.com/>

Ni dalali wa kujitegemea (*independent realtor*) wa nyumba, viwanja, mashamba, hoteli, shule na vituo vya mafuta jijini Dar es Salaam. Kama atakuwa hajihusishi na uandishi wa vitabu, utaalamu wa masoko basi atakuwa akijishughulisha na shughuli hii. Kupata huduma hii tembelea tovuti: <https://estateowners.wordpress.com/>

Pia ni mwandishi wa muswada wa show ya burudani, elimu na michezo cha iitwayo luninga **GAME ON**. Demo ya show iko [Youtube](#).

Kwa mrejesho umekionaje kitabu hiki, swali kuhusu huduma nilizotaja au ukitaka kuoda kitabu kingine

Piga simu: +255718515321/+255759694551

Barua pepe: rkilalile@gmail.com

KAZI ZINGINE ZA SHAMTE KILALILE

Vitabu vya Simulizi

1. [Nyuma ya Pazia la Utawa](#)
2. [Msaliti](#)
3. [Mpango Kabambe](#)

Vitabu vya Simulizi Fupi

1. Natamani Kukusahau
2. Isn't Such A Bad Idea

Vitabu vya Mahusiano & Mapenzi

1. Aina 8 Za Wanaume Zinazowavutia Wanawake (Kitabu cha Kwanza)

Miswada ya Filamu

1. [Nyuma ya Pazia la Utawa](#)
2. [Mpango Kabambe](#)
3. [100](#) (lugha ya Kiingereza)

Vitabu vya Biashara

1. [Personal Guide: How to Become an Entrepreneur](#)